



CHUSOMENI

KIBAJUNI

GIREDI 3

Yumna Hamid Titi

Fuad Aroi

Yumbe Athman



**TWAWEEZA
COMMUNICATIONS**
Working Towards a Better World

Shungwaya Welfare Association
Umaja ni Nguvu



SWAHILI RESOURCE CENTRE
*Old Town, Sir Mbarak Hisham Road
Mombasa*

Kimechapishwa na:

Twaweza Communications Ltd.
Jumba la Twaweza, Barabara ya Muthithi
Mpesi Lane
S.L.P. 66872 - 00800 Nairobi, Kenya
Simu: +(254) 020 269 4409; 0727 427740
Barua pepe: info@twavezacommunications.org
Wavuti: www.twavezacommunications.org

©Haki a kunakili nda Twaweza Communications
Chapisho la Kwanda 2024

ISBN: 978-9966-128-18-8

Kitabu cha Chusomeni Kibajuni ni sehemu a nradi wa kulindra na kuimarisha uṭamaduni wa Vabajuni. Nradi huu hutkeledhwa na kichuo cha Twaweza Communications, Shungwaya Welfare Association na Swahili Resource Centre. Undofadhiliwa na nfuko wa British Council Protection Fund kwa ushirikiano na Department for Digital, Culture, Media and Sport.

In partnership with



Yaliyomo

1:Vanyama Va Mwichuni	1
2: Usalama Barabarani	7
3: Kadhi Mbalimbali	12
4: Machumidhi A Mayi	16
5: Misimu Mbalimbali	21

SHUKURANI

Dhiṭabu dha *Chusomeni Kibajuni* ni sehemu a juhudi a kulindra na kuimarisha uṭamaduni wa Vabajuni. Chwatoa shukurani kwa mfuko wa British Council Protection Fund kwa nsaada ulochuwedhesha kuandika na kuchapisha dhiṭabu hidhi. Bila nsaada wavo ingalikuva ṭabu sana kuvapa vana va Kibajuni nafasi a kuifundrisha kusoma na kuandika Kibajuni. Chwavashukuru Dkt. Rukiya Harith na Nafisa Awadh kwa ushirikiano wavo na vaandishi kachika haṭua dhoṭe dha kuandika nfulululidho wa Chusomeni Kibajuni. Vaandishi va dhiṭabu hidhi – Yumna, Aroi na Yumbe – valiitolea kushiriki na kumalidha kuandika. Chwavashukuru sana kwa nchango huu muhimu. Pia twavashukuru vale voṭe chufanyao navo kadhi hii adwimu a kuhifadhi na kuimarisha uṭamaduni wa Vabajuni.

Kimani Njogu, Twaweza Communications
Omar Lali, Shungwaya Welfare Association
Athman Lali Omar, Swahili Resource Centre



Novemba, 2023

1

VANYAMA VA MWICHUNI

Kusikidha

Dhilio dha vanyama va mwichuni




Maagidho

- Mwalimu avasikidhishe vanafundi sauți mbalimbali dha vanyama na kuvavonesha video..
- Vanafundi vatabe sauți mbalimbali dha vanyama va mwichuni.

Kudhungumudha

Umuhimu wa vanyama va mwichuni



Kadhi a dhikundi

Vanafundi vadhungumudhe kuhusu umuhimu wa vanyama va mwichuni.

Kudhungumudha

Kulindra vanyama va mwichuni

Maagidho

Kachika dhikundri dhungumudhani kuhusu sampuli mbalimbali dha kulindra vanyama va mwichuni

Nfano:

- a) Vasivindwe.
- b) Vasiharibiwe makaadhi avo.

Kusoma

Kusoma



Hifadhi dha vanyama va mwichuni

Soma madhungumudho haa kisha ujibu maswali

- | | |
|------------|---|
| Mwalimu: | Huyambo asikari? |
| Asikari: | Siyambo mwalimu karibu kachika makaadhi a vanyama. |
| Mwalimu: | Asan̄ta |
| Asikari: | Mevona mevaecha vanafundi vavone vanyama va mwichuni |
| Mwalimu: | Nkweli asikari |
| Asikari: | Hamuyambo vanafundi karibuni kachika hifadhi a vanyama. |
| Vanafundi: | Hachuyambo, chumefurahi kuya hapa. |

- Asikai:** Mwapenda kuvona vanyama gani?
- Mwanafundi 1:** Napenda kunvona simba
- Mwanafundi 2:** Imi naṭaka kunvona nachi
- Asikari:** Ehhee! Hapa muṭavona vanyama voṭe va mwichuni
- Mwanafundi 3:** Nami naṭaka kunvona tuvi na pisi
- Asikari:** Bila wasiwasi muṭavavona vanyama voṭe.
- Mwanafundi 1:** Nina suwali, “Mbona hava vanyama vafundiwa na kulindrwa?”
- Asikari:** Hii ni ndia moyo a kuvalindra ili wasivuwawe na majangili
- Mwanafundi 4:** Mbona huvuwawa vanyama hava?
- Asikari:** Kuna sababu ḥingi dha kuvuwawa kama: kwa ajili a ḥama, ngodhi, pembe, meno na madoe. Pia kuna vachu vangine huvavuwa ili kuilindra ivo veneve na hondre dhavo dhisiharibiwe.
- Mwanafundi 5:** Kuna sababu ngine?
- Asikari:** Ndio, vanyama mwichu hupendedha vatalii na nchi echu hupacha sinti ḥingi dha kigeni.
- Mwanafundi 2:** Hae chupeke chuvavone havo vanyama.
- Asikari:** Chwendreni, ivani makini na muandike maina a vanyama voṭe muvavonavo.

Jibu masuwali

1. Vanafundi vamekwendra kwapi?
2. Ni vanyama gani valochaywa kachika madhungumudho haa?
3. Mwanafundi wa kwanda alipenda kumvona nnyama upi?
4. Andika sababu mbili dha kuvalindra vanyama mwichu.
5. Vavuo vanyama mwichu huichwae?

Kuandika

Kuundra senchensi

Maagidho

Apange maneno haa kuunda senchensi sawa

- a. mfalume ni simba mwichuni wa
- b. sana mbio ana tuvi
- c. alivamia muji simba
- d. ndrefu chiga una koo

Kadhi a dhiada

Chunga senchensi ukichumia maneno haa

- a. Jangili
- b. Mwichuni
- c. Nachi
- d. Vatalii

Kuandika

Kuchunga senchensi

Maagidho

Chunga senchensi tanu kuhusu ulindraji wa vanyama va mwichuni.

Kadhi a dhiada

Nraba

Tafudha maina a vanyama va mwichuni


N	S	H	K	M	P
Y	I	T	U	V	I
I	M	J	L	U	S
H	B	M	V	T	I
C	A	O	W	Y	V
A	D	R	X	O	M
N	A	C	H	I	A

2

USALAMA BARABARANI

Kusikidha

Hadisi



Maagidho

Kwa dhikundri vanafundi vatoleane dhisa kuhusu ajali dha barabarani.

Kudhungumudha

Shairi

Soma shairi hili kwa sauți

Huvaeledha ndrudhangu, maneno enye mashiko,
Usalama ni wa Mungu, lakini hadhari iko,
Chunga huumwi na ṭungu, nchocho shauri ako,
Usalama barabarani, chuuṭundeni muhimu.

Sharia dha chirafiki, ni muhimu dhiandamwe
Nvukaji huna dhiki, na husumbuliwi kamwe,
Kiyani kiviti ikiafiki, ṭaa a nehundru idhimwe.
Usalama barabarani, chuuṭundeni muhimu.


Pindri ikivaka redi, dereva komesha gari,
Yelo ikitaradadi, dereva keti ṭayari,
Kijani ndrio ahadi, nenda sasa ni shuari,
Usalama barabarani, chuuṭundeni muhimu.

Kuna dhebura kurosi, rangi a pundra milia,
Usiendreshe kwa kasi, gari lako pungudhia,
Ṭasababisha mikosi, kishaa ukiichia.
Usalama barabarani, chuuṭundeni muhimu.


Kusoma

Ufahamu

A




B




C



D



E



Sharia Dha Barabarani.

Ni ladhima kwa kila nchu kułukuwa ṭahadhari na kuva mwangalifu avukapo barabara. Wałakiwa kuva makini, kwani barabara si sehemu a kułedhewa. Uvukapo barabara wałakiwa kuangalia pandre dhołe mbili, kulia na kusoło ili kuhakikisha hakuna gari.

Sharia dha barabarani huchuekedha sehemu salama ambadho wawedha kuvuka, kwa nfano kuchumia daraja la kuvukia, kuvuka kwene alama dha pundra milia na kuangalia michoro a ṭahadhari.

Madereva wałakiwa vave vaangalifu sana. Ajali ningi husababishwa na madereva ambavo havako makini. Serikali ałakiwa kuvałukulia hałua kali dereva yoyote ałakaovunda sharia. Ni ladhima kwa kila dereva ave na leseni.

Magari maovu asikubaliwe kamwe kuchumika. Ni jukumu lechu isi kuwedha kunkomesha dereva aendeshao gari kwa mwendro wa kasi sana. Ivapo chutanyamaa, hwendra akasababisha ajali mbovu nno vachu vakapotędha maisha avo. Isi vołe chuvensi makini na vaangalifu. Barabara mbovu dhirekebishiwe ili kupungudha dhifo dhiłokeadho kila siku, chembelecho ajali haijali.

Maswali

1. Uvukapo barabara wałakiwa uve _____.
2. Uvukapo barabara wałakiwa kuangaliya pandre gani? _____
na _____
3. Ni sehemu gani salama dha kuvukia barabara? _____
4. Ni ladhima kila dereva ave na _____
5. Magari _____ asikubaliwe kuchumika..

Kusoma

Kusoma senchesi

Mukiva vavili vavili somani senchensi hidhi.

1. Usivuke mbee a magari a dharura.
2. Dereva nlevi alisababisha ajali.
3. Magari maovu aondrolewe barabarani.
4. Darajani ni sehemu salama a kuvukia
5. Usivuke kachikachi amagari aloegeswa.
6. Funga nshipi ukiva garini.
7. Vuka sehemu salama.
8. Dhifo dhingi husababishwa na ajali.
9. Usikimbie barabarani.
10. Usiṭedhe kachikachi a barabara.

Kuandika

Andika senchesi ukitumia maneno haa.

1. Kidhibiți mwendro
2. Ajali
3. Barabara
4. Dereva
5. Asikari

Kuandika

Kuandika nchungo

Andika nchungo nfupi kuhusu usalama barabarani.

3

KADHI MBALIMBALI

Kusikidha

Kadhi mbalimbali

Sampuli dha kadhi mbalimbali


A



B



C



D



Maagidho

Vanafundi vachaye kadhi mbalimbali dha kwechu.

Kudhungumudha

Kuṭaba

Vanafundi vatabe shuhuli dha kadhi mbalimbali vadhiyivadho.

Nfano

1. Vatabe mwalimu na mwanafundi
2. Dakitari na ngonjwa
3. Ntonyi na vanunudhi

Kudhungumudha

Shairi

Kadhi dha vadhee vechu, ni ḥingi kihadisia

Kuchema kukacha mwichu, mbeu iti vakichia

Kulima ni jadi echu, ndaa haikuchuvua.

Kwalikuva na vatonyi, isi vakichuechea

Vakiandroka mijini, baharini vakingia

Varudipo dhisiwani, isi mijini hwenea.

Vene kukacha boriti, ni kadhi a mashabiki

Makoko havaati, ndrio kupacha ridhiki

Kadhi dhiko sikititi, alo ndhivu haṭaki.

Sasa chuko masomoni, kadhi ḥingi ni muhimu

Dakitari na rubani, vanajeshi na valimu

Kwa bidii chusomeni, malengo echu atimu.

Maagidho

Soma na ukariri shairi hili kwa mahadhi.

Ufahamu

Uṭonyi



Uṭonyi ni moyo a kadhi itegemewao sana na vachu vaishivo karibu na bahari, ncho au idhiva. Kadhi a uṭonyi ni kadhi ihiṭajio uyudhi mwinci.

Vaṭonyi huṭoma kwa kuchumia ndia mbalimbali kama majarifa, nyavu, mayema, mishipi na juya. Ndia dhoṭe hidhi huṭoma isi ṭafauti ṭafauti. Vangine vakuru na vangine vadodi.

Vaṭonyi vendrapo baharini hupacha isi. Isi huchumiwa kama kichoveo na vangine hudhanywa vakapacha ridhiki dhavo. Pia isi husafirishwa nchi dha inde. Hii huchwechea sinti dha kigeni.

Mbali na kuṭoma isi, vaṭonyi pia huṭoma kamba, kaa na mayongoo. Hidhi ndridho dhenye sinti ningi, hudhanywa kwene mahocheli makuru na nchi dha inde.

Kadhi autonyi ni moyawapo wa kadhi kuru kwechu, lakini kuna kadhi mbalimbali na kila mmoya ana kadhi aipendao.

Jibu maswali

1. Vatonyi hutoma kwapi?
2. Chaya ndia chachu dha kutoomea.
3. Chaya faida mbili dha isi.
4. Mbali na isi, vatonyi hutoma nini kingine?
5. Uwe wapenda kadhi gani ukiva nkuru?

Kuandika

Imla

Maagidho

Sikidha kwa makini na uandike senchensi asomadho mwalimu.

Kuandika


Nchungo

Maagidho

Andika nchungo kuhusu kadhi uipendao.

Kusikidha

Machumidhi a mayi



Maagidho

Sikidha kwa makini hadisi utakaosomewa na mwalimu.

Kudhungumudha



Mwana: Huyambo mame?

Mame: Siyambo mwanangu

Mwana: Chupewa kadhi sikuli chuandike umuhimu wa mayi. Kwa nini mayi ni muhimu sana kwa vanadamu?

Mame: Mayi ni kiungo muhimu sana kwa vanadamu na pia kwa vanyama.

Mwana: Huchusaidiae isi vanadamu?

Mame: Huchasaidia kwa mambo mangi. Kwanda ni ladhima chunwe mayi kwa sababu mayi ni muhimu sana nvilini.

Mwana: Na je kupikia?

Mame: Kupikia pia ni muhimu. Huchumiwa pia kukoa, kufua nguvo, kuosa ɔnumba na mangine.

Mwana: Kuna umuhimu gani nngine mbali na machumidhi a ɔnumbani?

- Mama:** Huchumika sana hondreni, kwa vanyama na hata pia usafiri.
- Mwana:** Hondreni huchumika vipi?
- Mama:** Hondreni ni ladhima kuve na mayi ili kunosea mimea na kuvapa vanyama mayi kunwa. Pia huchumika kuosea dhifaa.
- Mwana:** Pia imi nilisomeshwa kachika isomo la sayansi kuva mayi huchumika kuenedha umeme.
- Mama:** Ni kweli mwanangu mayi ana machumidhi mangi.

Kusoma

Ufahamu

Mayi ni uhai

Mayi ni muhimu sana kwa maisha a mwanadamu. Bila a mayi hakuna uhai. Mayi ni tunu kutoka kwa Rabbi. Mola huchengedha ndia ḥingi dha kuchupa mayi. Asili a mayi ni vua. Kuna mayi a kisima, ncho, idhiva na bahari. Mayi ote hao ana umuhimu wake. Mayi huhifadhiwa kachika maṭangi, majabia , mapipa na vangine hufukua dhisima. Mayi haa huchumiwa kwa siku dha baadae hasa wakaṭi wa kiangadhi.

Mayi ana faidi ḥingi.Vanaḍamu huṭaka mayi a kukonga ruhu. Husaidia mivili echu kusaga chakula na kusafisha machumbo. Mwananḍamu hutakiwa aṇwe mayi bora wala sio bora mayi. Bila kudhingaṭia uswafi, mayi awedha kusababibisha maradhi kama kipindrupindru. Bila mayi hakuna uswafi. Mayi huchumika kusafisha nvili, nguvo na hata makaadhi echu. Mayi huchusafisha chukava swafi kama sufi.

Kuna dhakula ambadho hadhiliki ila dhipikwe hasa kwa kuchokosa. Kuna dhakula dha kuoka au kukanga nadho pia huhitaji mayi, ni ladhima dhioswe kabula a kupikwa. Mayi ni muhimu kachika upishi.

Kuna vanyama va mayini. Hava havawedhi kuishi bila a mayi nfano; isi, kamba, kiboko, kasa, pomboo na vanginevo. Kuna dhombo dha usafiri ambadho huchumia mayi nfano; meli, madau, majahadhi na michumbwi. Bila a dhombo hidhi, usafiri ungekuva shida sana dhisiwani.

Mayi huchumika wakați wa mikasa a mocho kudhinyia mocho. Vile vile kuna mashini ńingi ambadho huchumia mayi bila kusahau hondreni mambo haavi shuwari bila a mayi.

Jibu maswali

1. Bila a mayi hakuna _____
2. Mayi ni țunu kutoča kwa nyani? _____
3. Asili a mayi ni nini? _____
4. Chaya faida chachu dha mayi.
5. Toa mifano michachu a vanyama va mayini _____

Kusoma

Mesali

Soma misali hidhi kwa sauți

1. Hasira dha nkidi furaha kwa ntɔnyi.
2. Manahudha vangi idau hwendra nrama.
3. Jogoo wa hondreni haviki n'yini.
4. Fadhila dha pundra ni masheke.
5. Mayi akisuka haadholeki.
6. Nvumilivu hula mbivu.
7. Ntuma yuvani hula kivulini.
8. Mwendra omo țedhi hurudia ngamani.
9. Mwana akililia wembe mpe.
10. Haba na haba huyadha kibaba.

Kuandika

Umoya na wingi

Andika sentensi hidhi kwa wingi

Nfano: Mwana ndokunwa shai
Vana vandokunwa shai.

1. Fundi huundra jahadhi.

2. Nkulima alinosea mimea.

3. Idau lilidhama.

4. Nguvo indofuliwa.

5. Chombo kilioswa kwa udhuri.

6. Kisima kifukudhiwa.

7. Idovo likachisie kamba

Kuandika

Nchungo



Andika nchungo kuhusu machumidhi a mayi

5

MISIMU MBALIMBALI

Kusikidha

Misimu mbalimbali



Maagidho

Kachika dhikundri jadilianani kuhusu misimu mbalimbali kulingana na michoro.

Kudhungumudha

Njadala

Nsimu wa vua ni bora kuliko wa yuva.

Kusoma

Ufahamu

Misimu mbalimbali



Nsimu ni kipindri kachika mwaka ambapo hali maalumu a hewa hupachikana. Mabadiliko a hali a hewa kachika kipindri fulani cha mwaka hudhihirisha misimu mbalimbali. Misimu huirudia rudia kila mwaka. Kuna nsimu wa yuva ikali, nsimu huu mara ḥingi huva na **chaka** na upepo nkali, huichwa **kasikadhi**. Mimea na vanyama hudhoofika sana kwa kukosa mayi na chakula.

Nsimu nngine ni nsimu wa vua ḥingi, huu huichwa kusi. Vua ikidhidi nao husababisha **dhimba**. Vakulima hufurahia vua lakini isive a kupicha kiasi. Nsimu nngine ni nsimu wa **dhoruba**. Hapa upepo nkali huvonekana. Dhombi baharini hudhama. Vatonyi hukosa kwenda kuṭoma kwa kuhofia maisha avo na hasara a majahadhi kudhama.

Kuna nsimu nngine wa vua dha **rasha rasha**. Nsimu huu pia huva na baridi. Vua hii pia huichwa vua a kilimo. Dhichakwi hupachikanwa kwa wingi, vua hii ndio husaidia mimea kuchengedha dhakula. Kuna wakati nngine ambapo huva na upemo uvumao ku^loka **kusi na ma^lilahi** na vanavosafirisha dhombo baharini hutegemea pepo hidhi.

Jibu maswali

1. Eledha maana a nsimu.
2. Chaya aina a misimu kachika mwaka.
3. Ni nsimu gani vatonyi hushindrwa kwendra baharini?
4. Vakulima hufurahia nsimu upi?
5. Mariamu wendee sikuli uvadhie suecha. Wafikiri huu ulikuwa ni nsimu gani?

Kusoma

Kusoma senchesi

1. Kachika mwaka kuna misimu mbalimbali.
2. Vua ^lingi hunya nsimu wa kusi.
3. Upemo wa ma^lilahi ni ndhuri kusafirisha chombo.
4. Vua ikinya ^lingi husababisha dhimba.
5. Waka^li wa yuva ikali michi hukauka.
6. Upemo ukiva mwingi usendre baharini.

Kuandika

Nraba

K	I	A	N	G	A	D	H	I
B	S	M	K	C	K	H	D	L
C	K	L	U	H	G	O	S	R
R	D	K	S	A	Y	R	W	A
H	E	W	I	K	F	U	T	H
M	A	T	L	A	I	B	N	D
V	R	O	J	U	V	A	J	V

Maagidho

Chumia nraba kujibu maswali afuachao.

1. Nsimu wa vua ዓንግዴ ነው _____
2. Ni nsimu gani mimea hukauka? _____
3. Wakati wa kiangadhi huwa እና ብቻ? _____
4. Ni nsimu gani vatonyi hushindwa kwendra ቅመልማት? _____
5. Upopo gani manahudha hupenda kusafiria? _____

Kuandika

Kuandika nchungo

Maagidho

Andika nchungo kuhusu shuhuli mbalimbali dhifanyikadho wakati wa misimu mbalimbali a mwaka.